210mm x 200mm

FOLD FOLD FOLD FOLD

## Utangulizi

Makala haya ya ushauri yanakusudia kuwasaidia watumiaji wa huduma za posta na utumaji wa vifurushi katika kutayarisha na kufunga vifurushi vya posta ili kuhakikisha kwamba vimefikishwa kwa njia salama kupitia kwa mitandao ya posta/ utumaji wa vifurushi.

## Ufungaji

Vifurushi vya posta huwa na maumbo na ukubwa tofauti, kwa hivyo ni muhimu kwa watumiaji kutambua ufungaji vifurushi unaofaa, ulio na nafasi ya kutosha, uliositiriwa vyema kwa ndani ili kudhibiti vifurushi vya posta.

Sheria ya Kenya ya Habari na Mawasiliano SURA ya 411 A ya 1998 huchukulia vifurushi vya posta visivyofungwa kwa njia ifaayo kuwa marufuku hasa vikiwa navifaa vilivyochongoka ambavyo havijadhibitiwa vizuri ili kuzuia kuumia kwa mtu yeyote au kuharibiwa kwa vifurushi vingine vya posta vinaposafirishwa kwa kutumia njia hiyo ya posta.

Mtu anaweza kutumia aina mbalimbali za vifaa vya kufungia vifurushi tokea bahasha (za barua, nyaraka, n.k.) hadi masanduku na vyombo vingine vya kuwekeavifaa kulingana na ukubwa, uzito na umbo la kifurushi cha posta.

## Pahali pa kupata vifaa vifaavyo vya kufungia

Unaweza kununua maboksi yaliyo na ukubwa tofauti katika takriban maduka yote makuu na maduka mengine ya rejareja. Pia unahitaji kujua ni aina gani ya leseni inayotoa vifaa vya kufungia bila gharama zaidi, au pia kwa kulipa ada fulani kupitia kwa viungo vya nyavuti za watumiaji, nyingine ambazo huweza kupatikana katika wavuti wa Mamlaka ya Mawasiliano ambao ni www.ca.go.ke

Unashauriwa kutumia vifaa vya kufungia ambavyo havijatumiwa awali kufungia vifurushi vya posta. Pale ambapo matumizi ya vifaa kama hivyo hayawezi kuepukika, mtumiaji lazima azibe maandishi ya anwani ya awali katika kifaa hicho cha kufungia.

## Ufungaji wa Vifurushi vyako vya Posta

### Kudhibiti kifurushi

Dhibiti vifurushi vyako kwa kutumia magazeti ya zamani, sponji au karatasi zilizochanwa, mbali na vifaa vingine. Pale ambapo boksi au kifaa cha kuwekea vifaa kimefungwa, lazima kitingishwe ili kuhakikisha kwamba kilichomo kimesitiriwa vizuri. Kusogea kwa vifaa vilivyomo katika boksi/ kifurushi kunaashiria uhitaji wa udhibiti zaidi.

### Kutuma vifaa vinavyoweza kuvunjika upesi kwa njia ya posta

Kama unaweza kupata sponji ya plastiki au kitu cha kukinga, kitumie ili kulinda vifaa vyako kwa kuweka vifaa hivyo kwa kuvikinga ndani ya uwazi ulio katika vifaa unavyotuma pia. Weka alama yenye kuashiria "Vya kuvunjika" au weka alama "Kuharibika upesi" katika vifurushi vilivyo na chakula au vitu vingine vinavyoweza kuharibika. Ufungaji wa uangalifu ndiyo njia nzuri ya kulinda vifaa vyako vya thamani dhidi ya uharibifu.

### Kutuma vifaa vizito kwa njia ya posta

Iwapo unatuma kitu kizito sana au chenye uzito, anza kwa kutumia boksi imara, funga vifaa kwa usalama kwa kutumia kikazio chenye nguvu ili kuzuia kutikisika, kisha weka utepe kwenye kona zote. Hakikisha umezingatia uzito unaoruhusiwa.

### Kuziba

Kwa kutumia utepe unaoweza kuona upande mwingine au wa rangi ya hudhurungi, ulio imara au utepe wa karatasi, funga kifurushi chako cha posta kwa njia inayofaa. Usitumie kamba, uzi, kitani, utepe wa kuzibia au wa plastiki kufungia kifurushi chako cha posta.Kuweka utepe unaoweza kuona upande mwingine juu ya anwani yako kutasaidia anwani hiyo dhidi ya kuchafuka au hata kutoka. Pale ambapo utumaji unahusisha utumaji wa vifurushi kimataifa au kupitia kwa huduma ya utumaji ya posta, watumaji wanapaswa kutangaza yale yaliyomo katika vifurushi vinavyofungwa kupitia kwa mtoa huduma wa posta/utumaji wa vifurushi ili kuthibitisha vitu ambavyo vimefungwa. Kwa hivyo, ni vyema vitu hivyo kufungwa katika eneo la posta/utumaji wa vifurushi, mahali ambapo vitu hivyo vimefikishwa ili kutumwa.

## Kuandika anwani

Anwani ya upokeaji wa kifurushi huweza huandikwa kwenye upande ulio mrefu wa kifurushi, na maandishi yawe makubwa kuweza kusomeka kwa urahisi. Usitumie vituo au nukta katika anwani na hakikisha umetumia nambari maalum za posta husika *(codes)* kwa usahihi, ambazo pia zinaweza kupatikana kwa wakuu wa posta au kutoka katika wavuti wa PCK ambao ni www.posta.co.ke

Watumaji pia lazima waweze kujua iwapo kitu wanachotaka kutuma ni marufuku kwa kuulizia kutoka kwa mkuu wa posta au pia kutalii wavuti wa mtoa huduma. Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya (CA) pia imetoa maelezo kuhusu matumizi yafaayo ya anwani za posta ambazo hupatikana kupitia kwa kiungo cha wavuti kinachohusu mtumaji

kupitia www.ca.go.ke

Anwani ya marejeshokurudisha kwa aliyetuma kwa kawaida huandikwa kwenye sehemu ya juu ya kushoto katika upande uo huo ulio na anwani ya kutuma kifurushi. Kuweka pia anwani ya kutuma pamoja na ile ya kurudisha kwa aliyetuma marejesho ndani ya kifurushi chenyewe kutahakikisha kwamba mzigo huo utawasilishwa ipasavyo endapo kibandiko chenye anwani ya nje kitaharibiwa au hata kuanguka. Pale ambapo vifaa vilivyotumiwa kufungia kifurushi vitatumika tena, maandiko na vibandiko vyote vya awali havina budi kuondolewa au kufutwa kabisa kwa kutumia kalamu ya wino mweusi.

## Utumaji

Hakikisha kwamba umeweka stempu za kutosha katika kifurushi chako ili kuzuia kuchelewa au kutofikishwa kwa kifurushi. Mtoa huduma wa posta/utumaji wa vifurushi atakataa kukubali na kutuma vituvitu vyako kupitia kwa posta bila malipo hayo. Ikiwa kifurushi chako kina uzani wa gramu 350 au chini yake na umeweka stempu sahihi, unaweza kukitumbukiza ndani ya sanduku la barua la posta katika eneo hilo. Kwa upande mwingine, unaweza kuwasilisha kifurushi chako kwa mtoa huduma za posta/utumaji wa vifurushi utakayemchagua kulingana na mahitaji yako.



## Unahitaji kufahamu zaidi?

Kwa habari zaidi kuhusu mada iliyopo hapo juu au sehemu nyingine yoyote ya afya na usalama wa mitambo ya mawasiliano, tafadhali wasiliana na:

COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA


**Head Office**
CA Centre, Waiyaki Way, P.O. Box 14448, Nairobi 00800
Mobile: 0703042000,
Complaints: chukuahatua@ca.go.ke
Talk to us : pea@ca.go.ke
020-445 5555, 0714 455 555, 0737 455 555

**CA Western Regional Office**
1st Floor KVDA Plaza
P.O. Box 2346
Eldoret 30100
Mobile: 0703042105
Email: wro@ca.go.ke

**Central Regional Office**
Ground Floor, Advocates Plaza
P.O Box 134
Nyeri 10100
Mobile : 0703042181
Email : cero@ca.go.ke

**CA Coast Regional Office**
3rd Floor, NSSF Building
P.O. Box 8041
Mombasa 80100
Mobile: 0703042152
Email: cro@ca.go.ke

**Nyanza Regional Office**
2nd Floor Lake Basin Mall,
P.O Box 2016
Kisumu 40100
Mobile: 0703042130
Email: nro@ca.go.ke



**Ilani ya kujitoa hatarini:** Huku kila jaribio likiwa limefanywa ili kuhakikisha kuwa habari iliyojumuishwa katika hati hii ni sahihi, imekusudiwa TU kuwa kama mwongozo wa kuelekeza utendakazi salama wa mitambo ya mawasiliano na haipaswi kuchukuliwa kama (au kutumika badala ya) ushauri wa kisheria. Kwa hivyo,

Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya haitakubali kosa lolote kwa matokeo ya hatua zozote zilizochukuliwa, au maamuzi yaliyotolewa kwa misingi ya taarifa iliyotolewa.



CA/PEA/CEP/KIS/B/14/2020


COMMUNICATIONS AUTHORITY OF KENYA

www.ca.go.ke

# VIDOKEZO KUHUSU UFUNGUAJI VIFURUSHI VYA POSTA



kaa macho